# AZIMIO LA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU

*Azimio kuhusu Haki na Wajibu wa Watu, Makundi na Mihimili ya Jamii katika Kukuza na Kulinda Uhuru na Haki za msingi za Binadamu zinazotambulika kiulimwengu.*

09.12.1998

TAREHE YA KUPITISHWA KWA AZIMIO. AZIMIO LILIPITISHWA TAREHE

AZIMIO LILIPITISHWA KWA MARIDHIANO YA MKUTANO MKUU WA UMOJA WA MATAIFA

## WATETEZI NI AKINA NANI?

Wanaume na wanawake ambao wanaolinda na kutetea haki za binadamu, kwa mfano wale wanaotetea uhuru wa kujieleza, haki za wanawake, wazawa, makundi ya pembezoni na watu wenye jinsia tata. Wanaweza kuwa watetezi binafsi au kupitia mashirika ya utetezi.

## JE, UNAWEZAJE KUWAUNGA MKONO WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU?

- Sambaza taarifa juu ya Azimio la watetezi wa haki za binadamu
- Changia katika utambuzi wa kazi za watetezi wa haki za binadamu
- Unga mkono mashirika ambayo husaidia na kulinda watetezi wa haki za binadamu
- Saidia watetezi waliopo kwenye hatari
- Kuwa mtetezi wa haki za binadamu! Kila mtu ana haki, na wajibu, wa kukuza na kutetea haki za binadamu

## JE AZIMIO LINAELEZEA NINI?

Azimio limejikita katika, linajumuisha na lina akisi nguvu ya sheria za kimataifa zinayohusika na ukuzaji, ulinzi na utetezi wa haki za binadamu.

## HAKI NA ULINZI KWA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU

- KUKUZA HAKI ZA BINADAMU KATIKA NCHI ZAO NA DUNIANI KOTE
- TETEA HAKI ZA BINADAMU PEKE YAKO AU NA WATU WENGINE
- KUUNDA JUMUIYA AU MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI
- KUKUTANA AU KUKUSANYIKA KWA AMANI
- KUTAFUTA, KUPATA, KUPOKEA NA KUWA NA TAARIFA ZINAZOHUSIANA NA HAKI ZA BINADAMU
- KUENDELEZA NA KUJADILI MAWAZO MAPYA YA HAKI ZA BINADAMU NA KANUNI NA KUTETEA ILI ZIKUBALIKE
- KUWASILISHA KWA WENYE MAMLAKA KASORO NA MAPENDEKEZO KWAAJILI YA KUBORESHA UTENDAJI WAO NA KUWAONYA JUU YA TISHIO LOLOTE KUHUSU KUTAMBUA HAKI ZA BINADAMU
- KUTOA MALALAMIKO JUU YA SERA RASMI NA VITENDO VINAVYOHUSIANA NA HAKI ZA BINADAMU NA KUONA MALALAMIKO HAYO YANAPITIWA
- KUTOA MSAADA WA KISHERIA KIKAMILIFU AU USHAURI MWINGINE NA MSAADA KATIKA UTETEZI WA HAKI ZA BINADAMU
- KUHUDHURIA MIKUTANO YA UMMA, KESI MBALIMBALI ILI KUTATHMINI UZINGATIAJI WA WAJIBU WAKE KATIKA SHERIA ZA KITAIFA NA KIMATAIFA KUHUSU MAJUKUMU YA UTEKELEZAJI WA HAKI ZA BINADAMU
- KUWASILIANA BILA KIZUIZI CHOCHOTE NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI YA KITAIFA NA KIMATAIFA.
- KUPATA FIDIA STAHIKI
- KWA UTENDAJI HALALI WA KAZI AU UTAALAMU WA MTETEZI WA HAKI ZA BINADAMU
- KWA ULINZI BORA CHINI YA SHERIA YA KITAIFA WAKATI WA KUPINGA UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU
- KUSHAWISHI, KUPOKEA NA KUTUMIA RASILIMALI KWA LENGO LA KULINDA HAKI ZA BINADAMU

ARTICLES 1, 5, 6, 7, 8, 9, 11, 12 AND 13

## MAJUKUMU YA NCHI

- KULINDA, KUKUZA NA KUTEKELEZA HAKI ZOTE ZA BINADAMU
- KUHAKIKISHA KWAMBA WATU WOTE CHINI YA MAMLAKA YAKE WANAWEZA KUFURAHIA HAKI ZOTE ZA BINADAMU UHURU WA MSINGI
- KUPITISHA HATUA ZA KISHERIA, KIUTAWALA NA HATUA ZINGINE ILI KUHAKIKISHA UFANISI WA UTEKELEZAJI WA HAKI NA UHURU
- KUTOA FIDIA STAHIKI KWA WATU WANAODAI KUATHIRIKA NA UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU
- KUFANYA UCHUNGUZI USIO NA UPENDELEO KWA HARAKA WA MADAI YA UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU
- KUCHUKUA HATUA ZOTE MUHIMU ILI KUHAKIKISHA ULINZI WA KILA MTU DHIDI YA VURUGU YOYOTE, VITISHO, ULIPIZAJI KISASI, UBAGUZI, SHINIKIZO AU KITENDO CHOCHOTE KILE KAMA MATOKEO YA KAZI ZAO ZA HAKI ZA BINADAMU
- KUKUZA UFAHAMU KWA UMMA KUHUSU HAKI ZA KIRAIA, KISIASA, KIUCHUMI, KIJAMII NA UTAMADUNI
- KUHAKIKISHA NA KUUNGA MKONO UANZISHAJI NA MAENDELEO YA TAASISI HURU ZA HAKI ZA BINADAMU
- KUKUZA NA KUWEZESHA MAFUNDISHO YA HAKI ZA BINADAMU KATIKA NGAZI ZOTE RASMI ZA ELIMU NA MTAALAMU MAFUNZO

ARTICLES 2, 9, 12, 14 AND 15

## MAJUKUMU YA KILA MTU

- KUKUZA HAKI ZA BINADAMU, KULINDA DEMOKRASIA NA TAASISI ZAKE NA SIO KUKIUKA HAKI ZA BINADAMU WENGINE
- WATU WANAOFANYA KAZI KWA TAALUMA ZAO AMBAO WANAWEZA KUATHIRI HAKI ZA BINADAMU WENGINE, HASA MAAFISA WA POLISI, WANASHERIA, MAHAKIMU, MAJAJI, NK WANAJUKUMU LA KULINDA HAKI HIZI

ARTICLES 10, 11 AND 18

*Kwa habari zaidi tembelea : **www.protecting-defenders.org***

Design by Oh ! Ilaliss